



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



### UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA ZANZIBAR

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, inawatangazia wananchi wote kuwa, Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na mzunguko wa sita utafanyika Zanzibar kuanzia tarehe 07 hadi 13 Oktoba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kila kituo katika Mikoa yote mitano ya Zanzibar.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatatu tarehe 07 Oktoba, 2024 hadi tarehe 13 Oktoba, 2024 siku ya Jumapili.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Shehia zote katika mikoa yote mitano ya Zanzibar.
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

Uboreshaji unahusisha: -


1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 lakini pia hawana sifa ya kuandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha, Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupiga kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume [www.inec.go.tz](http://www.inec.go.tz) au anuani ya [ovrs.inec.go.tz](http://ovrs.inec.go.tz) kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

### MAMBO YA KUZINGATIA

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika katika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRs kwa kupiga \*152\*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua Namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao wameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), wapiga kura ambao walioandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA, NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 03 Oktoba, 2024 na:

  
Grayson A. Orcado

**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**